Je, watoto wetu wanajifunza?

Utafiti wa uwezo wa watoto kusoma na kuhesabu Tanzania 2010[1]

Utangulizi

Kote nchini, maendeleo makubwa yamefikiwa kwenye elimu ya msingi ndani ya muongo (miaka 10) uliopita. Uandikishaji umepanda maradufu kote elimu ya msingi na sekondari, na mamilioni ya watoto wameweza kwenda shule. Tanzania iko mbele ya muda wa kutekeleza na kuyafikia malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs) yanayohusu upatikanaji wa elimu na usawa wa kijinsia katika elimu. Madarasa maelfu yamejengwa na maelfu ya walimu wameajiriwa. Bajeti ya elimu imeongezeka mara tatu zaidi kwa kipindi hiki; Serikali sasa inatumia dola za kimarekani zaidi ya bilioni moja kila mwaka au karibu Sh 1 kwa kila Sh 5 ya bajeti ya elimu.

Mafanikio haya siyo hatua rahisi; yalihitaji dhamira kubwa ya kisiasa na mgawo mkubwa wa fedha za umma. Wazazi pia wamejitahidi kugharamia sehemu yao, maana hata ile elimu ya bure kiuhalisia sio bure, maana kuna gharama za sare za shule, vitabu, kalamu, masomo ya ziada, usafiri na mengineyo. **Swali la msingi hapa ni – Je, jitihada na uwekezaji huu mkubwa umezaa matunda gani? Je, watoto wetu wanauwezo wa kusoma na kufanya mahesabu?** Mantiki ya elimu ni kumsaidia kila mtoto kukuza maarifa ili aweze kuishi maisha yenye ustawi ndani ya dunia – kwa kuanza kujua kusoma na kufanya mahesabu stadi ambazo zinaweka msingi wa uwezo wa kudadisi, kufikiri, kusikiliza, kuuliza maswali, kuchambua, kupambanua na kuwasiliana kwa kujiamini. Je, shule zetu zinafanikiwa kwenye jukumu hili? Watoto wetu wanajifunza?

Juhudi ya *Uwezo* imeundwa kujibu swali hili muhimu, na ripoti hii inawasilisha matokeo ya utafiti wake wa kwanza. *Uwezo* ni juhudi ya miaka minne inayofuatilia ubora wa

---

[1] Muhutasari huu umeandaliwa na Uwezo Tanzania (www.uwezo.net). Uwezo iko ndani TEN/MET (www.tenmet.org) na ni sehemu ya juhudi pana ya Afrika Mashariki inayoratibiwa na Twaweza (www.twaweza.org)

ujifunzaji mashuleni kwa kupima uwezo wa watoto wenye umri kati ya miaka 5 na 16 kusoma na kufanya hesabu kwa wanafunzi. Juhudi hii nchini Tanzania iko ndani ya TEN/MET (Mtandao wa Elimu Tanzania, www.tenmet.org); na ni sehemu ya juhudi pana ya Afrika Mashariki ukizijumuisha pia nchi za Kenya na Uganda inayoratibiwa na Twaweza (www.twaweza.org). Upimaji umezingatia mbinu bora iliyothibitika iliyoandaliwa na Kituo cha ASER nchini India, na inatumia mbinu ya kisayansi kupata sampuli nasibu ya kaya nchi nzima. Watafiti waliopatiwa mafunzo walizitembelea kaya na kupima stadi za kusoma (Kiswahili na Kiingereza) na kufanya Hisabati kwa kila mtoto kwa kutumia jaribio fupi la ngazi ya darasa la 2. Ngazi ya darasa la 2 imechaguliwa kwa sababu kwa mujibu wa viwango vya kimataifa na Tanzania hadi kufikia mwisho wa mwaka wa pili wa elimu ya msingi kila mtoto anapaswa kuwa tayari ana stadi za msingi za kujua kusoma na kufanya hesabu.

Upimaji wa kwanza wa *Uwezo* nchini Tanzania ulifanyika Mei 2010, baada ya maandalizi makubwa na upimaji wa majaribio. Ulihusisha wilaya 38 kati ya wilaya 133 za Tanzania. Katika kila wilaya vijiji 30 vilichaguliwa kwa nasibu, na katika kila kijiji watoto wote wenye umri kati ya miaka 5-16 katika kaya 20 walipimwa. Kwa ujumla, watoto 42,033 katika kaya 22,800 walipimwa uwezo wao katika stadi za msingi. Matokeo sita muhimu ya upimaji huo yanawasilishwa hapa chini. Ripoti kuu inaweza kuchukuliwa hapa www.uwezo.net

Matokeo Muhimu

1. Mhitimu mmoja kati ya wahitimu watano hawezi kusoma Kiswahili cha ngazi ya darasa la 2



Japo Kiswahili ni lugha inayozungumzwa kwa upana zaidi nchini, idadi kubwa ya watoto hawawezi kusoma Kiswahili bila shida. Kwenye sampuli zetu, chini ya nusu (42.2%) ya watoto waliofanyiwa uchunguzi waliweza kusoma kwa hatua ya hadithi. Wakati watoto wote katika darasa la 3 wanapaswa kuweza kusoma hadithi ya ngazi ya darasa la 2, watoto chini ya mmoja kati ya 3 (32.7%) ndio wanaweza. Watoto wengi hawajifunzi kusoma hadithi rahisi hadi wafikie darasa la 5 au la 6. Hata hivyo, hadi wanamaliza shule ya msingi, mtoto mmoja kati ya 5 hawezi kusoma hadithi ya ngazi ya darasa la 2. Licha ya kumaliza miaka saba ya elimu ya msingi, watoto hao wanaelekea kubaki mbumbumbu (hawajui kusoma na kuandika) maishani mwao.

ASILIMIA YA WATOTO WANAOWEZA KUSOMA KISWAHILI NGAZI YA DARASA LA 2						
Darasa	**Hajui kitu**	**Herufi**	**Neno**	**Aya**	**Hadithi**	**Jumla**
Awali	53.5	27.7	2.7	2.5	13.6	100
Darasa la 1	41.8	37.8	10.6	4.2	5.6	100
Darasa la 2	24.1	32.3	17.0	9.8	16.8	100
Darasa la 3	14.8	20.0	16.4	16.1	32.7	100
Darasa la 4	9.6	14.7	12.0	16.6	47.1	100
Darasa la 5	6.0	10.1	7.4	13.8	62.8	100
Darasa la 6	4.0	6.1	4.9	11.1	73.9	100
Darasa la 7	1.8	5.9	3.3	8.0	81.0	100
Jumla	18.6	19.2	9.6	10.5	**42.2**	100

2. Nusu ya wanafunzi hawawezi kusoma Kiingereza cha ngazi ya darasa la 2



Kiingereza ni somo gumu zaidi kwa wanafunzi. Ingawa wanafunzi wote wa darasa la 3 wanapaswa kuweza kusoma Kiingereza cha ngazi ya darasa la pili, chini ya mwanafunzi 1 kati ya 10 (7.7%) ndio anaweza. Maendeleo kwenye somo la Kiingereza ni ya taratibu sana; kwa darasa la tano, ni mtoto 1 tu kati ya watoto 4 anaweza kusoma hadithi. Karibu nusu ya wanafunzi hawawezi kusoma hata maneno mafupi ya Kiingereza. Watoto wengi wanafika darasa la 7 bila kuwa na stadi zozote za Kiingereza. Hadi wanamaliza shule ya msingi, nusu ya wanafunzi (49.1%) bado hawawezi kusoma hadithi ya kiwango cha darasa la 2 ya Kiingereza, na bila shaka wanafunzi wachache sana wanauwezo wa kusoma kwenye ngazi ya darasa la 7. Hii ina maana kuwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaoingia sekondari hawawezi kusoma kwa lugha ya Kiingereza, ambayo ni lugha ya kufundishia elimu ya sekondari.

ASILIMIA YA WATOTO WANAOWEZA KUSOMA KIINGEREZA NGAZI YA DARASA LA 2						
Darasa	**Hajui kitu**	**Herufi**	**Neno**	**Aya**	**Hadithi**	**Jumla**
Awali	68.3	16.9	2.3	3.4	9.1	100
Darasa la 1	68.0	24.8	3.8	1.3	2.1	100
Darasa la 2	55.5	29.4	7.5	3.8	3.9	100
Darasa la 3	42.0	26.7	14.2	9.4	7.7	100
Darasa la 4	29.0	24.0	16.0	15.5	15.4	100
Darasa la 5	21.4	19.6	13.7	20.9	24.5	100
Darasa la 6	15.1	13.6	13.6	21.9	35.8	100
Darasa la 7	7.9	11.5	10.7	19.1	50.9	100
Jumla	37.8	21.0	10.4	12.1	**18.7**	100

3. Wahitimu 7 tu kati ya 10 wanaweza kufanya hesabu za ngazi ya darasa la 2



Ingawa stadi za kuzidisha ziko kwenye mtaala wa darasa la 2, wanafunzi wachache tu wa darasa la 2 waliweza kuzidisha bila shida. Zaidi ya nusu ya wanafunzi hawawezi hata kujumlisha. Hadi kipindi wanafika darasa la 5, watoto wengi wanaweza kutoa na kujumlisha, lakini wengi bado hawawezi kuzidisha. Watoto wengi wanapata stadi za Hisabati mwishoni mwa shule ya msingi. Hata hivyo, watoto 3 kati 10 (31.5%) wa darasa la 7 bado hawawezi kufanya hesabu za kuzidisha za ngazi ya darasa la 2. Na mtoto 1 kati ya 10 anamaliza shule ya msingi bila kuwa na stadi za Hisabati kabisa; hawezi hata kujumlisha hesabu ndogo. Hii inaweza kumaanisha kuwa watoto wengi wanaojiunga na shule za sekondari hawana msingi imara kwenye Hisabati ambao ni muhimu kwenye ujifunzaji na uchambuzi, hasa katika masomo ya sayansi na biashara.

ASILIMIA YA WATOTO WANAOWEZA KUFANYA HISABATI NGAZI YA DARASA LA 2								
Darasa	**Hajui kitu**	**Namba**	**Kujumlisha1**	**Kujumlisha2**	**Kutoa1**	**Kutoa2**	**Kuzidisha**	**Jumla**
Awali	40.0	41.9	2.7	1.6	1.7	1	11.0	100
Darasa la 1	26.5	56.9	9.2	1.9	2.3	1	2.4	100
Darasa la 2	15.7	45.8	16.9	4.9	5.5	4	7.6	100
Darasa la 3	9.9	30.3	20.0	8.5	7.3	6	18.5	100
Darasa la 4	7.2	22.0	14.1	10.0	7.0	7	32.8	100
Darasa la 5	5.1	13.9	11.0	10.3	6.7	7	45.8	100
Darasa la 6	3.3	9.2	7.7	10.2	5.9	6	57.8	100
Darasa la 7	2.2	7.9	4.8	7.0	4.7	5	68.5	100
Jumla	13.1	28.3	11.1	7.0	5.2	5	**30.8**	100

4. Watoto wa mijini hufanya vizuri zaidi kuliko wa vijijini

Watoto wa mijini hupata asilimia kati ya 7 na 10 zaidi kuliko watoto wa vijijini katika masomo yote. Tofauti ni kubwa zaidi hususani katika madarasa ya 2-4, wakati watoto wa mijini huanza kupata stadi za msingi ilhali wenzao wa vijijini wanaachwa nyuma. Inaelekea kuwa watoto wa vijijini hatimaye huanza kupata stadi hizo za darasa la pili wafikapo madarasa ya 6 na 7; lakini kuna uwezo mkubwa kuwa wanazidi kuporomoka zaidi kwenye stadi ya kusoma katika ngazi yao



5. Wasichana hufanya vizuri kuliko wavulana

Wasichana walifanya vizuri zaidi katika masomo yote waliyopimwa, ingawa tofauti ni ndogo sana. Kati ya watoto wote waliopimwa, 43.5% ya wasichana waliweza kusoma hadithi katika Kiswahili ikilinganishwa na 40.7% ya wavulana. Katika masomo ya Kiingereza na Hisabati tofauti ilikuwa ni ndogo mno, kama inavyooneshwa katika jedwali hapo chini. Hata hivyo matokeo haya yanapingana na ile dhana ya muda mrefu

kuwa wasichana hawafanyi vizuri kama wavulana, na inaibua maswali kuhusu kwa nini kunakuwa na tofauti kubwa katika matokeo ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ambapo wavulana hung'ara zaidi. Hata hivyo, tofauti hizi ndogo zisifiche ule ukweli mkubwa zaidi kuwa watoto wengi mno wasichana na wavulana hawana uwezo wa kimsingi katika masomo ya lugha zote mbili na Hisabati.



6. Watoto wenye mama waliosoma hufanya vizuri zaidi

Watoto ambao mama zao wamesoma hadi elimu ya sekondari hufanya vizuri sana kuliko watoto wengine. Kwa mfano, katika darasa la 3 na 4 watoto hawa wana uwezekano wa *mara tano zaidi* kuweza kusoma hadithi ya Kiingereza na wana uwezekano wa *mara mbili zaidi* kufanya Hisabati na kusoma hadithi ya Kiswahili. Hata watoto ambao mama zao wamemaliza elimu ya msingi tu wanafanya vizuri kiasi kuliko wale ambao mama zao hawajasoma kabisa. Tofauti katika matokeo huanza kujionesha kuanzia darasa la kwanza hadi darasa la saba; ikiashiria kwamba elimu ya mama ni muhimu katika ngazi zote za shule.



Hitimisho

Matokeo ya tathmini ya *Uwezo* iliyohusisha kaya zaidi ya 20,000 na watoto zaidi ya 40,000 yanaonesha kuwa kuna tatizo kubwa katika elimu nchini Tanzania. Hadi wanapoingia darasa la 3, watoto asilimia 100% wanapaswa kuwa na stadi za kusoma na kuhesabu. **Lakini ukweli ni kuwa hadi darasa la 3, watoto 7 kati ya 10 hawawezi kusoma Kiswahili cha msingi; watoto 9 kati ya 10 hawawezi kusoma Kiingereza cha msingi, na watoto 8 kati ya 10 hawawezi kufanya Hisabati za msingi**.

Hata wanapofikia hatua ya kumaliza elimu ya msingi idadi kubwa mno ya watoto huwa hawawezi kufanya kile ambacho walipaswa kuwa wana kijua miaka mitano iliyotangulia wakati wakiwa katika darasa la 2. Mgawanyo kiwilaya unaonesha tofauti kubwa kati yao, na ambapo baadhi ya wilaya ziko chini sana ya wastani wa kitaifa.

Ukweli ulio bayana ni kuwa, licha ya maendeleo makubwa yaliyofikiwa katika elimu yaliyowezekana kutokana na kuwekezwa kwa matrillioni ya shilingi kila mwaka, idadi kubwa sana ya watoto nchini Tanzania hawajifunzi.

Je, nini kifanyike kuhusu hali hii?

Kwanza, tunahitaji kutulia na kutafakari matokeo haya na kuchunguza yanamaanisha nini. Kukimbilia kuyapuuza au kutunga masuluhisho ya haraka haraka pengine haitasaidia, kwani inaweza kusababisha kushindwa kutambua kiini cha tatizo na hivyo kuchukua hatua zisizofaa. Kushangilia majengo mapya na idadi kubwa ya watoto wanaoandikishwa shule inaweza kuwa hatari kama matokeo yake ni kufunika ukweli kwamba idadi kubwa ya watoto wanamaliza elimu ya msingi bila kujua kusoma na kuhesabu.

Pili, ingawa changamoto lazima ziwepo pale ambapo mfumo wa elimu unapopanuliwa ghafla, bado tunaweza kuuliza: Je, mikakati ya kisera na malengo ya kisiasa yanalenga mambo sahihi? Hivi sasa, nchini Tanzania na kwingineko, mkazo zaidi umewekwa katika kupatikana kwa vitendeakazi kama vile madarasa, maabara, vitabu na walimu, badala ya matokeo ya ujifunzaji. Mathalani, stadi za kusoma, kuhesabu, kuandika udadisi na ubunifu. Kwa vile ushahidi unaonesha kuwa vitendeakazi havijaleta stadi hizi, kuna umuhimu wa kupanga mfumo mzima wa elimu kulenga zaidi uwezo na stadi za mwanafunzi, kuanzia ndani ya wizara zinazohusika na elimu, taasisi za elimu, watunga mitaala, mitihani, tathmini ya walimu na shule, vipimo vya maendeleo na vipaumbele vya kisiasa.

Tatu, kuna haja ya kuangalia zaidi nini kinachotokea shuleni kuliko kutazama takwimu za kitaifa pekee. Tafiti zilizofanyika katika nchi nyingi zinaonesha kuwa mchakato wa kufundisha na kujifunza unaweza kuwa na hitilafu kubwa. Mawili kati ya matatizo ambayo hujitokeza mara kwa mara ni kuwa shule hazipati fedha za kutosha (yaani bajeti za elimu zinazoongezeka zinatumika kwa mambo mengine badala ya kuboresha shule) na kwamba walimu hawana motisha ya kutosha na hawafundishi (yaani muda wanaotumia kufundisha darasani ni mdogo mno). Pengine itasaidia kuchambua mambo hayo mawili

kwa kina, na kutafuta namna ya kuyaboresha. Pia kuna haja ya kuangalia kwa makini uhusiano kati ya rasilimali za kutosha kufika shuleni na walimu kuwapo kazini kwa upande mmoja, na uwezo na stadi za mwanafunzi anapohitimu kwa upande mwingine.

Nne, uwazi zaidi unaweza kuwawezesha watunga sera na watu wengine kutafakari na kuchukua hatua. *Uwezo* imedhamiria kusambaza matokeo ya tafiti zake ili kusaidia kulifikia lengo hili. Lakini Serikali inaweza kwenda mbele zaidi ili kuwezesha data za kila shule kupatikana kwenye mtandao, na katika vyombo vya habari kila afisa wa serikali ya mtaa, mwalimu, mzazi na mwanafunzi alinganishe hali na utendaji wake na wa wengine. Maendeleo ya teknolojia hasa usambazaji wa simu za mkononi vimewezesha ubadilishanaji habari katika kiwango kikubwa na kufungua fursa mpya nyingi.

Tano, badala ya kuendelea kufanya kile ambacho kimeshafanyika kwa jitihada zaidi, pengine umefika wakati wa kufanya kitu tofauti. Utafiti wa *Uwezo* na tafiti zilizofanyika duniani zinaashiria kuwa kiini cha kitendawili hiki ni kuangalia upya suala la motisha ili wadau muhimu katika sekta hii watambuliwe kwa kuhamasisha kujifunza. Wazo moja ambalo linafaa kufikiriwa, na ambalo Rais Jakaya Kikwete kesha lipokea, linaitwa *cash on delivery* au *malipo baada ya matokeo* (www.cgdev.org/section/initiatives/active/codaid). Msingi wake mkuu ni kuwa kupatikana kwa fedha zaidi kwa kazi ya elimu kutategemea kufikiwa kwa malengo (yaliyokaguliwa na shirika huru), kama vile kusoma na kuhesabu (kwa mfano kwa kila mtoto anayemaliza elimu ya msingi akiwa na stadi zilizokubalika, zitatolewa Sh laki tatu). Wazo hili linaweza kupanuliwa ili hizo Sh laki tatu zigawiwe kwa viongozi wa eneo ilipo shule, walimu, na pengine hata wazazi. Lengo ni kuwashawishi wadau wahusika kuzingatia na kutambua mafanikio katika kujifunza. Hakuna hakikisho kuwa wazo hili litafanikiwa. Lakini katika hali ya kuwepo kwa tatizo kubwa linaloikabili sekta ya elimu Tanzania kwa sasa, hasa pale ambapo njia za kawaida zimeshindwa kuleta mafanikio ya maana, kufanya majaribio mbadala yaliyofikiriwa kwa makini kama hii ya *malipo baada ya matokeo*, na kisha kuchunguza matokeo yake inaweza kutusaidia kusonga mbele.

Matokeo ya utafiti wa *Uwezo* yanazinduliwa katika kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu nchini Tanzania. Vyovyote matokeo ya siasa yatakavyokuwa, miaka mitano ijayo inatoa fursa ya kulitazama sakata la elimu kwa uwazi, ujasiri na kwa njia itakayoleta mafanikio. Ni watu wenye stadi, uwezo na wanaojiamini watakao liwezesha taifa letu kuneemeka hususani katika muktadha wa ushirikiano wa Afrika Mashariki na katika hali ya utandawazi. Yeyote atayechaguliwa kuwa Rais ajaye wa Tanzania, kazi ya kuibadili elimu kutoka kuangalia vitendeakazi hadi kuhakikisha kila mtoto anaweza kusoma na kuhesabu na kujifunza pengine ndicho kitakuwa kipimo kikuu cha mafanikio ya uongozi wake.